



## **AZIMIO NA. 6/2018**

### **AZIMIO LA BUNGE LA KUMPONGEZA MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWA JITIHADA NA MAAMUZI MBALIMBALI YA KUWAINUA WANANCHI WANYONGE HASA WAKULIMA WA KOROSHO NA WAKULIMA WA MAZAO MENGINE**

---

**KWA KUWA**, tatizo la bei na masoko ya uhakika ya mazao mbalimbali katika nchi yetu lilikuwa limeota mizizi na kuendelea kuathiri maendeleo ya wakulima wetu hapa nchini. Mathalani tatizo la kukosekana kwa masoko na bei nzuri ya mazao mbalimbali limekuwa likilalamikiwa na wakulima wa mazao mbalimbali wakiwemo wakulima wa zao la Mahindi, Kahawa, Mpunga, Mbaazi, Ufuta, Alizeti, Korosho na mazao mengine yanayolimwa kwa wingi katika nchi yetu;

**KWA KUWA**, tatizo la bei ndogo za mazao na ukosefu wa masoko ya uhakika limekuwepo hapa nchini kwa muda mrefu bila kuchukuliwa hatua madhubuti na za dhati katika kukabiliana na tatizo hilo;

**KWA KUWA**, suala la bei ndogo za mazao wakati mwingine huwa ni mpango wa wafanyabiashara wachache kuwadhulumu haki wakulima wetu wanaotumia jasho jingi katika kuzalisha mazao husika. Ni ukweli usiopingika kwamba, katika uchumi wa soko unaondeshwa na watu wachache wenye nguvu ya fedha, upo

uwezekano mkubwa wa baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa na uzalendo na hofu ya Mungu kutumia umaskini wa wakulima wetu kuwadhulumu haki ya kupata bei stahiki za mazao yao kwa visingizio mbalimbali ikiwemo kisingizio cha kushuka kwa bei ya zao husika katika soko la dunia;

**NA KWA KUWA**, Mhe. Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imetambua changamoto ya bei ndogo za mazao ya wakulima wetu na kuamua kuitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali. Mathalani tumekuwa tukishuhudia Mheshimiwa Rais akitoa maelekezo na miongozo mbalimbali ya namna Serikali yake inavyopaswa kuwatafutia masoko wakulima wake;

**KWA KUWA**, Mheshimiwa Rais wetu ameendelea kufanya na kuchukua hatua mbalimbali za kupigania bei nzuri na masoko ya uhakika ya mazao ya wakulima wetu;

**KWA KUWA**, jitihada hizo zinaonekana na zinaleta faraja na neema kubwa kwa wakulima wetu hapa nchini. Mathalani, juzi tarehe 12 Novemba, 2018, Mheshimiwa Rais wetu aliamua kusitisha ununuzi wa zao la Korosho kwa njia za minada baada ya kutoridhishwa na mwenendo wa ununuzi wa zao hilo kwa bei zilizopangwa na wafanyabiashara. Mathalani, iliripotiwa kwamba, msimu huu wa 2018 wafanyabiashara wa Korosho walipanga kununua Korosho kwa bei ya Shilingi 2500 kwa kilo moja tofauti na bei ya zaidi ya Shilingi 3500 kwa kilo moja ya Korosho ghafi iliyotumika kwa msimu uliopita wa 2017;

**KWA KUWA,** Mheshimiwa Rais hakuridhishwa na mwenendo na bei ya zao hilo na kuamua Serikali kununua Korosho zote zinazozalishwa na wakulima wetu kwa bei ya zaidi ya shilingi 3300 kwa kilo moja ya Korosho ghafi;

**NA KWA KUWA,** uamuzi huo umeweza kuokoa fedha za wanyonge zaidi ya Bilioni 160 za Kitanzania iwapo Korosho zilizopo ambazo ni zaidi ya Tani 200,000 zingenunuliwa kwa bei ya Shilingi 2500 kama ilivyopendekezwa na wafanyabiashara;

**KWA KUWA,** uamuzi aliofanya Mheshimiwa Rais umelenga katika kuwaondoa wakulima wetu katika minyororo ya unyonyaji na ulanguzi uliokuwa umekithiri katika nchi yetu. Na kwa kuwa uamuzi huo utaleta tija kwa wakulima wetu na uchumi wa nchi kwa ujumla;

**KWA HIYO BASI,** Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Tatu, Kikao cha Saba, tarehe 14 Novemba, 2018, linaazimia kwa kauli moja kama ifuatavyo:-

- (i) Kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumuunga mkono kwa uamuzi wake wa kuamua kusitisha ununuzi wa zao la Korosho kwa bei ya kinyonyaji na kuelekeza Korosho zilizopo zinunuliwe na Serikali kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa fedha zitakazotolewa na benki ya Kilimo kwa bei ya Shilingi 3300 kwa kilo moja ya Korosho ghafi;

- (ii) kuiomba Serikali kuchukua hatua za makusudi na za haraka kutafuta masoko ya uhakika kwa mazao mengine kama vile Pamba, Pareto, Kokoa, Katani, Mahindi, Mchele, Kahawa, Mbaazi, Ufuta, Alizeti na mazao mengine yanayozalishwa kwa wingi katika nchi yetu ikiwezekana kuchukua hatua kama zilizochukuliwa katika zao la Korosho;
- (iii) Serikali iimarishe uwezeshaji wananchi kupitia utaratibu wa kuyaongezea mazao yetu thamani kwa kuyachakata hapa hapa nchini ili kupanua wigo wa ajira kwa wananchi wetu hususan vijana wetu;
- (iv) Kuwaomba watazania wakiwemo wafanyabiashara, wafanyakazi, wakulima, wavuvi na wafugaji kuendelea kuipa ushirikiano Serikali yetu inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kuwaletea maendeleo kwa ufanisi na kwa haraka zaidi.

**Limepitishwa na Bunge leo tarehe 15 Novemba, 2018**

Stephen Kagaigai  
**KATIBU WA BUNGE**